

wanarudi kwenye maeneo yao kulala," wengi tofauti miaka mingine hususana Iringa na kumalizia mkoani Mbeya.

SHERIA

MWANANCHI UK 10

# \*Wafugaji wakaidi kukiona\*

**Askari wa wanyamapori wamekuwa wakifanya kazi kwa kufuata sheria za nchi**

Habel Chidawali, Mwananchi  
hchidawali@mwananchi.co.tz

Dodoma. Serikali imewaonya wafugaji wanaoingiza mifugo yao hifadhini kuacha kujichukuliwa sheria mikononi wanapokamatwa, kwa kile ilichoeleza kuwa polisi hawatasita kutumia nguvu kujilinda na kuwakamata wahalifu.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk Hamisi Kigwangalla wakati akijibu swali la mbunge wa viti maalumu (Chadema), Roda Kunchela aliyetaka kujua iwapo Serikali inatambua idadi ya wafugaji waliopata madhara ikiwamo vifo, uonevu, mifugo kutaifishwa na kutozwa faini zinazokuka sheria za nchi.

Mbunge huyo pia, alihoji Serikali

inachukua hatua gani kwa baadhi ya askari wanyamapori wanaofanya uonevu unaokiuka sheria mbalimbali kwa wafugaji nchini.

Waziri Kigwangalla alisema kwa nyakati tofauti, wafugaji ambao wamekuwa wakiingiza mifugo yao ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa wamekuwa wakikamatwa na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Alisema utaratibu unaotumika kuwakamata wafugaji hao mara zote unazingatia sheria na taratibu zinazosimamia maeneo ya hifadhi na wala si kuvunja sheria.

Dk Kigwangalla alisema askari wa wanyamapori wamekuwa wakifanya kazi zao kwa kufuata sheria za nchi katika ulinzi wa rasilimali za Taifa.

Alisema Serikali imekuwa ikitoa msisitizo kwa watumishi hao kufuata sheria na taratibu katika kuwakamata wale wote wanaoingiza mifugo ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa ikiwa ni

pamoja na kuwafikisha katika vyombo vya sheria.

"Katika ukamataji wa wahalifu hao, taratibu za kisheria zinafuatwa, hata hivyo, kwa nyakati tofauti kumekuwa na matukio ya wafugaji kuvamia vituo vya askari na kuwashambulia kwa silaha za jadi kwa lengo la kuchukua mifugo yao suala ambalo ni kinyume na sheria za nchi," alisema Dk Kigwangalla.

Alitolewa mfano kuwa katika Hifadhi ya Taifa Ruaha mnamo Oktoba, 9, 2018 askari wanyamapori mmoja ali-uawa na wananchi waliovamia Kituo cha Nyota kwa lengo la kukomboa mifugo yao iliyokuwa imekamatwa baada ya kuingizwa katika hifadhi hiyo kinyume na utaratibu.

Julai 3, 2016 askari mwingine wa wanyamapori ali-uawa na wananchi waliovamia Kituo cha Ikoga kwa lengo la kukomboa mifugo yao jambo alilosema halikubariki.

**"Kwa nyakati tofauti kumekuwa na matukio ya wafugaji kuvamia vituo vya askari na kuwashambulia kwa silaha za jadi kwa lengo la kuchukua mifugo yao suala ambalo ni kinyume na sheria za nchi."**

Dk Kigwangalla

ASKARI

Corona